**KIAMBATISHO**

**MAAZIMIO YA KIKAO KAZI CHA WENYEVITI NA WATENDAJI WA TAASISI ZA UMMA, KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO YA KIMATAIFA CHA ARUSHA, TAREHE 19 HADI 21 AGOSTI, 2023**

## 1. KUHUSU MAGEUZI KWENYE TAASISI ZA UMMA

(i) Kwamba, kila Taasisi iwe na mkakati madhubuti unaoakisi maono na agenda ya mabadiliko ya uendeshaji na utendaji wa Taasisi za umma.

(ii) Kwamba, Taasisi za Umma ziongeze ufanisi katiza uzalishaji na utoaji huduma na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Mfuko wa Serikali Kuu.

(iii) Kwamba, mpango wa kuziunganisha Taasisi zenye majukumu yanayo shabihiana na kuingiliana, uzingatie utaratibu wa kisheria na ushirikishwaji wa wadau wote wanaohusika, kulinda ajira na stahili za watumishi pamoja na mali za umma.

(iv) Kwamba, Taasisi za Umma zinazofanya biashara zifanye tathmini na zile zenye uwezo ziuze hisa zake kwenye soko la hisa kuwapa wananchi nafasi ya kuwa na umiliki.

## 2. KUHUSU UENDESHAJI WA TAASISI

(i) Kwamba, Taasisi za Umma zizingatie usalama wa Serikali katika uendeshaji wa shughuli zake.

(ii) Kwamba Taasisi za Umma ziwekeze katika kujenga uwezo na kuendeleza rasili-mali watu kwa kutoa kipaumbele kwenye akili hisia *(emotional intelligence).*

(ii) Kwamba, Taasisi zilizopewa uhuru wa kujiendesha zihakikishe masuala ya ajira yanafanyika kwa mujibu wa sheria na bila upendeleo *(nepotism)*

(iii) Kwamba, kuhusu vigezo vya mikataba ya utendaji kazi vilivyowasilishwa na Msajili wa Hazina, Taasisi ziwasilishe mapendekezo ya kuboresha vigezo hivyo;

(iv) Kwamba, Msajili wa Hazina azisaidie Taasisi za umma kudhibiti matumizi yake hususan kwenye suala la kutakiwa kugharamia shughuli za Wizara mama;

(v) Kwamba, Taasisi za Umma ziwe na Mawasiliano ya kimkakati na ziwekeze katika kujenga na kukuza chapa (branding); na

(vi) Taasisi zibainishe maeneo ya ushirikiano badala ya kuendeleza ushindani usio na tija.

## 3. KUHUSU USIMAMIZI

(i) Kwamba, utambuzi na utoaji tuzo za Msajili wa Hazina kwa Taasisi za umma usizingatie kigezo cha fedha pekee na faida pekee, bali maboresho ya mifumo ya kutoa huduma kwa Taasisi zinazotoa huduma;

(ii) Kwamba, Msajili wa Hazina ahakikishe Taasisi zote za Umma zinaingia Mikataba ya Utendaji Kazi na kuzifanyia tathmini. Aidha, taarifa za tathmini zitumike katika kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusiana na usimamizi wa Taasisi;

(iii) Kwamba Taasisi za Umma ziimarishe matumizi sahihi ya TEHAMA katika uendeshaji na utoaji huduma; na

(iv) Watendaji Wakuu wafanye maandalizi stahiki kabla ya kukutana na Kamati za Bunge kwa kuzingatia kuwa Taasisi ni sehemu ya Serikali hivyo zinapaswa kutoa maelezo ya kina ya shughuli zake pamoja na namna ambavyo mmejipanga ku-wahudumia wananchi.

## 4. KUHUSU MASUALA MAHSUSI YA UCHUMI

(i) Kila Taasisi iwe na mkakati madhubuti wa kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, ama kupunguza uagizaji vitu nje ya nchi; na

(ii) Taasisi za Umma ni nguzo muhimu ya utekelezaji wa mipango ya nchi. Kwa msingi huu, kila Taasisi inapaswa kuwianisha mipango na miradi yake na Dira ya Maende-leo ya Taifa.